Powered by: www.manyamfranchise.com

JINA_____KIDATO_____

TAREHE _____ SAHIHI _____

KISWAHILI
KIDATO CHA KWANZA
MUHULA WA PILI 2015
SAA 2½ .

Cheti Cha Kuhitimu Elimu Ya Secondari Nchini Kenya
KISWAHILI
KIDATO CHA KWANZA MUHULA WA PILI 2015

Maagizo:

- ***Jibu maswali yote katika sehemu zilizoachwa wazi kwa kutumia Kiswahili sanifu.***
- ***Makosa ya tahajia na sarufi yataadhibiwa.***
- ***Mtihani huu una alama 90***

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

	UPEO	TUZO
INSHA	20	
UFAHAMU	20	
LUGHA	50	
FASIHI	10	
JUMLA	100	

Mtahiniwa ahakikishe kwamba karatasi hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa

Powered by: www.manyamfranchise.com

Sehemu I: Insha (alama 20)

Mwandikie mwalimu mkuu wa shule yako barua ukimwelezea malalizo mnayokumbana nayo shuleni.

Powered by: www.manyamfranchise.com

Sehemu II: Ufahamu (alama 20)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:

Uzuri mwema nyumbani, si uzuri wa mlango,
Wala si dirishani, ulopambwa kwa mpango,
Uzuri ni ulo ndani, ndipo liwepo ni jengo,
Nyumba njema si mlango, fungua uone ndani.

Hata unapoiamba, ukajenga kwa mpango,
Ukaitia mabamba, katu hilo si jingo,
Pambo la nje ya nyumba, ni nakshi ya uwongo,
Nyumba njema si mlango, fungua uone ndani.

Hata kuta ziwe kombo, viambaza vya majengo,
Bora ni la ndani pambo, ndipo yawapo majengo,
Si hoja la nje umbo, japo ndani kuna pengo,
Nyumba njema si mlango, fungua uone ndani.

Na sasa nawaambia, nyumba yake madhumuni,
Uzuri ulotimia, si uzuri wa usoni,
Wala si wa kuvalia, nguo rasmi mwilini,
Nyumba njema si mlango, fungua uone ndani.

Awe ni mtu mchafu, na kivazi kilo ndani,
Tena awe na harufu, anuka hawezekani,
Atapata Utukufu, kwa sifa njema mwilini,
Nyumba njema si mlango, fungua uone ndani.

Kaditamati shairi, mawili tuyapimeni,
Umbo na roho nzuri, kipi aula jamani?
Ni moyo wenye fahari, kwa uzuri na imani,
Nyumba njema si mlango, fungua uone ndani.

Maswali:

a) Lipe shairi ulilosoma kichwa mwafaka. (alama 2)

_____

_____

_____

b) Mshairi ana maana gani kwa kusema 'nyumba njema si mlango, fungua uone ndani'? (alama 2)

_____

_____

_____

c) Shairi hili lina beti ngapi? (alama 1)

_____

d) Eleza vina katika ubeti wa nne (alama 2)

_____

_____

e) Eleza mizani katika ubeti wa pili mshororo wa tatu (alama 1)

_____

_____

Powered by: www.manyamfranchise.com

f) Taja na ueleze kituo cha shairi hili ni cha aina gani (alama 2)

g) Toa mifano miwili ya mbinu ya Inkisari kama ilivyotumiwa na mshairi (alama 2)

h) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)

i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili (alama 4)

Mabamba

ii) Nakshi

iii) Viambata

iv) Fahari

sehemu III: Matumizi ya Lugha (alama 50)

a) taja sifa mbilimbili zinazotambulisha irabu zifuatazo (alama 2)

i) /e/

ii) /u/

Powered by: www.manyamfranchise.com

b) Tambua mzizi katika vitenzi vifuatavyo (alama 2)

i) Alitukaribisha

ii) Wametuchezea

c) Onyesha silabi katika neno: daftari (alama 2)

d) Tunga sentensi tatu ili kuonyesha matumizi tofauti ya kitone (.) (alama 3)

e) Andika nomino zozote zenye sauti zifuatazo (alama 2)

i) Kiyeyusho cha kaakaa ngumu

ii) Kipasuo-kikwamizo

f) ~~Tambua neno lenye [illegible] katika neno: inayojenga~~ (alama 3)

Bainisha aina ya mgeuno katika sentensi hii'.

Hiki kimeletwa hapa na mtoto wake.

g) Akifisha sentensi ifuatayo (alama 3)

ah mbona unamsukuma mwenzio shangazi aliuliza

Powered by: www.manyamfranchise.com

h) Taja aina zozote mbili za insha (alama 2)

i) Eleza maana mbilimbili za vitawe vifuatavyo (alama 4)
i) Kanga

ii) Panda

j) Onyesha nomino katika sentensi ifuatayo (alama 3)
Jana Shangazi alinunua marashi na kifurushi cha vipodozi sokoni.

k) Andika visawe vya (alama 2)
i) Dua

ii) Bi. Kizee

l) Sahihisha (alama 2)
Kitabu ambacho nilichosoma ni cha kusisimua

m) Kanusha (alama 3)
i) Amekuwa akisinzia tangu asubuhi.

ii) Walituazima Vitabu vyao.

Powered by: www.manyamfranchise.com

iii) Ukinipendeza nitakuajiri.

n) Taja aina zozote tatu za maktaba (alama 3)

o) Eleza maana ya: (alama. 1)
i) Kiimbo

ii) Shadda (alama. 1)

p) Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika nyakati/ hali ulizopewa katika mabano (alama 4)
i) Kuku na bata wengi waliuzwa (ujao)

ii) Nyanya anatuchemshia mahindi. (uliopita, hali timilifu)

iii) Wanasiasa wamchutubu mikutanoni. (mazoea)

iv) Mwimbaji ataimba wimbo mzuri. (uliopita)

q) Tumia kiunganishi mwafaka kukamilisha sentensi zifuatazo. (alama 3)
i) Sikula wali.....mchuzi.

ii) Tutajitahidi.....tupite mtihani huu.

iii) Nilifua nguo..... nikaenda sokoni.

r) Kamilisha tashbihi zifuatazo (alama 3)
i) Siku hizi Chiriku amepoa kama .....

Powered by: www.manyamfranchise.com

ii) Halima ni mwoga kama .....

iii) Tajiri huyo ana tumbo kubwa kama .....

s) Andika kwa ukubwa (alama 2)
i) Mbwa wanang'ang'ania makombo

ii) uliofurika jana usiku Mto

Sehemu IV: Fasihi (alama 10)

a) Eleza maana ya fasihi (alama 2)

b) Taja tanzu mbili kuu za fasihi (alama 2)

c) Fafanua dhima za fasihi katika jamii (alama 6)